

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Simu: 255 22 2460735/2460706-8
Faksi: 255 22 2460735/2460700
Barua pepe: met@meteo.go.tz
Tovuti: www.meteo.go.tz



P.O. BOX 3056
DAR ES SALAAM

Unapojibu tafadhali nakili:

Kumb Na: TMA/3000/5/Vol II

23 Machi, 2017

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI NA WADAU WOTE

YAH: MAADHIMISHO YA SIKU YA HALI YA HEWA DUNIANI
TAREHE 23 MACHI, 2017

Kila mwaka ifikapo tarehe 23 Machi nchi wanachama 190 wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani hujiunga kuadhimisha kuzaliwa kwa Shirika hilo lililoanzishwa tarehe 23 Machi, 1950 kulingana na kauli mbiu teule. Kauli mbiu ya mwaka huu ni *'Tuyaelewe mawingu na umuhimu wake'* (*Understanding clouds*).

Katika kuadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani (WMD), Shirika la Hali ya Hewa Duniani limetambua umuhimu wa kuongeza uelewa wa mawingu ili kujua zaidi mchango wake katika mzunguko wa maji kati ya nchi kavu, baharini na angani na uhusiano wake na hali ya hewa ya muda mfupi na mrefu. Kama inavyojulikana kuwa mawingu yana umuhimu mkubwa sana katika mifumo ya hali ya hewa ya dunia na hivyo elimu juu ya tabia ya mawingu itasaidia katika kutabiri hali ya hewa na kutambua mabadiliko ya tabia nchi kwa wakati ujao. Wahenga huwa wanasema, *Dalili ya Mvua ni Mawingu*.

Kama ilivyo kwa wanachama wengine, Tanzania inaungana nao kuadhimisha siku hii inayofikia kilele leo tarehe 23 Machi, 2017 kwa kuwakaribisha wananchi wote kutembelea vituo vya hali ya hewa nchini ili kuona shughuli zitolewazo na Mamlaka na kujifunza. Aidha, Mamlaka itambelea na kutoa elimu kwa vijana wa baadhi ya shule na vyuo mbali mbali nchini kupitia ofisi zake zilizopo nchi nzima. Kutoa makala za siku

hiyo kwenye magazeti, vipindi kwenye radio, televisheni na mitandao ya kijamii kuhusu elimu juu ya mawingu na sayansi hali ya hewa kwa ujumla, hii itasaidia kuongeza wigo wa elimu kwa umma hususani mashuleni.

Tunawatakia maadhimisho mema ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani

'Tuyaelewe mawingu na umuhimu wake'
(Understanding Clouds)